Toleo 74 - Shaaban 1444 H / Machi 2023 M

# Jarida la UQAB

# Je, KHILAFAH INASIMAMISHWA VIPI?

#TurudisheniKhilafah

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

حزب التحرير HIZB UT TAHRIR

KUMB: 06/1444 Ijumaa, 26 Rajab 1444 H 17/02/2023 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Hizb ut Tahrir / Kenya Yaandaa Maandamano Baridi kwenye Kumbukumbu ya Miaka 102 ya Kuanguka kwa Khilafah

Kama sehemu ya kumbukumbu ya miaka 102 tokea kuvunjwa kwa Khilafah, Hizb ut-Tahrir Kenya iliweza kuandaa maandamano baridi baada ya swala za Ijumaa mnamo tarehe 17 Februari 2023 M sambamba na tarehe 26 Rajab 1444 H.

Maandamano haya yalikusudiwa kukumbusha Umma hali tete inayoendelea kukumbana nayo tokea kuangushwa kwa Khilafah tarehe 28 Rajab 1342 H, sawa na tarehe 3 Machi,1924. Tokea tukio hili la kuhuzunisha, umma wa Kiislamu umegawanywa kupitia mradi wa kikoloni wa Sykes-Picot uliopelekea pia ardhi zao kukaliwa kimabavu na kutawaliwa na ukoloni. Damu za Waislamu zikimwagwa huko Syria, Yemen na China bali katika nchi zote za Kiislamu, hali inayoonesha kiwango kikubwa cha maumivu umma unayopitia. Mtetemeko wa ardhi hivi karibuni huko Uturuki, ardhi ambayo Khalifah wa mwisho alifukuzwa kufuatia mkataba wa khiyana wa Lausanne umeonesha kiwango cha juu cha utepetevu cha serikali za ulimwengu wa Kiislamu. Leo kwa hakika walimwengu wote wanakumbwa na hali ngumu ya kiuchumi, uongozi fisidifu na maovo ya kijamii kama natija ya kuvunjwa kwa Khilafah.

Huku idadi ya Waislamu ikikurubia bilioni 2, lakini idadi hii imekuwa mithili ya povu la bahari kwa kutoweka kwa Khilafah mlinzi na ngao ya Waislamu. Umma wa Kiislamu umekosa heshima, utukufu na mlinzi. Umepoteza kibla chake cha kwanza katika biladi tukufu ya Isra wal Miiraj. Na ni kwa kupitia Khilafah pekee ndio kibla hiki pamoja na biladi zilizokaliwa na Wamagharibi zitarudishwa mikononi mwa Waislamu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) atusimamishie kwa haraka Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, Naye Mwenyezi Mungu ni Muweza wa jambo lake lakini watu wengu hawajui.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari wa Hizb ut-Tahrir Kenya**


Pepe: info@uqab.or.ke




Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, na rehma na amani zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, na jamaa zake, na Maswahaba zake, na waliomfuata.

Kwa Ummah wa Kiislamu, kwa jumla… na kwa wabeba Da'wah kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah Rashida, hasa…

Katika siku hii, tarehe 28 Rajab mwaka 1342 H, sawia na tarehe 3 Machi mwaka 1924 M, yaani, miaka 102 ya Hijria iliyopita, makafiri wakoloni, wakiongozwa na Uingereza wakati huo, wakishirikiana na wasaliti wa Kiarabu na Kituruki, waliweza kuiondoa dola ya Khilafah. Mustafa Kemal alitekeleza jinai ya ukafiri wa wazi, kwa kuiondoa Khilafah huko Istanbul, huku akimzingira Khalifa, na kumpeleka uhamishoni katika majira ya mapema siku hiyo. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Msiba huu mchungu ulitokea, kwa kuvunjwa Khilafah, ndani ya Ardhi za Kiislamu... Ilikuwa ni faradhi juu ya Ummah kupigana na yule anayetekeleza ukafiri wa wazi kwa upanga, kama ilivyosimuliwa katika Hadith iliyopokewa na Bukhari na Muslim ya Mtume (saw), kutoka kwa Ubada ibn al-Samit (ra), «وَأَنْ لَا نُنَازِعَ الْأَمْرَ أَهْلَهُ إِلَّا أَنْ تَرَوْا كُفْراً بَوَاحاً عِنْدَكُمْ مِنْ اللهِ فِيهِ بُرْهَانٌ» **"Na tusizozane na wenye mamlaka isipokuwa mukiuona ukafiri ulio wazi ambao mnao ushahidi wa wazi mbele ya Mwenyezi Mungu."** [Bukhari na Muslim] Hata hivyo, Ummah haukufanya chochote kumtingisha mhalifu huyo na wasaidizi wake, kiasi kwamba yeye na washirika wake wangegeuzwa kuwa wenye hasara. Badala yake, jibu lilikuwa dhaifu na halikuwa karibu na hilo!

Hapo ndipo historia ya Ummah ilipotiwa giza. Hapo awali, Khilafah ilikuwa ni dola ya Ummah, iliyosimama juu ya haki na uadilifu lakini sasa Ummah una zaidi ya vijidola hamsini, vyenye madhara makubwa kutoka kwa watawala wao. Hata tetemeko la ardhi la Syria na Uturuki, katikati ya mwezi huu wa Hijri wa Rajab, halikuweza kuondoa mgawanyiko wao, na kuregesha umoja wa dola moja. Badala yake, waliendelea kama vipande vilivyopasuka, kabla na baada ya tetemeko la ardhi, wala hawakujali! Amesema Mwenyezi Mungu (swt), ﴿أَوَلَا يَرَوْنَ أَنَّهُمْ يُفْتَنُونَ فِي كُلِّ عَامٍ مَرَّةً أَوْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ لَا يَتُوبُونَ وَلَا هُمْ يَذَّكَّرُونَ﴾ **"Je! Hawaoni ya kwamba wanatiwa mtihanini kila mwaka mara moja au mara mbili? Kisha hawatubu, wala hawakumbuki."** [Surah At-Tawba 9:126].

Hata hivyo, janga la tetemeko hili la ardhi lilidhihirisha kwamba Uislamu umekita kwa kina ndani ya Waislamu. Walipokuwa wakiwaokoa ndugu zao kutoka chini ya vifusi, Waislamu walipiga takbira. Takbira hazikukoma katika ndimi zao, hasa walipokuwa wakimuokoa mtoto mchanga ambaye mama yake alimzaa, kisha akafa chini ya kifusi... ama yule ambaye alifinikwa na kifusi, huku mkono wake ukionekana umeshika tasbihi, ambayo kwayo alikuwa akimtukuza Mwenyezi Mungu (swt)... au walipokuwa wakijaribu kumtoa mwanamke kutoka chini ya jengo lililobomoka, mwanamke huyo aliomba afinikwe kichwa chake, kabla ya kutolewa nje, ili nywele zake zisionekane au pale yule aliyeita kutoka chini ya kifusi ili atolewe, aliomba kwanza maji ya kutawadha kabla ya swala ili wakati wa kuswali usimpite... kisha yule waliyekuwa wakijaribu kumuokoa kutoka katikati ya vifusi, na wakamkuta anasoma Surat Al-Baqarah ndani ya Quran ... au msichana ambaye walikuwa wanajaribu kumtoa, ambaye anaelezea huzuni yake kwa sababu hakuweza kuswali siku hiyo ... wakati wote huo, takbira zilisikika, Allahu Akbar... Hawa ndio Waislamu. Mwenyezi Mungu (swt) amrehemu kila Muislamu aliyefariki wakati wa tetemeko la ardhi. Wawe miongoni mwa mashahidi wa Akhera, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt). Mwenyezi Mungu (swt) awaponye waliojeruhiwa, kwa tiba isiyoacha maradhi nyuma… Mwenyezi Mungu (swt) amnusuru kila Muislamu aliyesalimika. Mwenyezi

***Endelea... UK 4***

Mungu (swt) amjaalie maisha mema, ayatumie katika kumtii Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wake (saw)...

Hawa ndio Waislamu, ilhali hao ndio watawala katika Ardhi za Kiislamu. Kwa kweli wametofautiana mbingu na ardhi. Pengo hili la utofauti lilitokea katika kipindi hiki cha miaka 102 Hijria, tangu msiba mkubwa wa kuondolewa kwa Khilafah! Kisha, kwa kupatiliza kuanguka kwa Khilafah, makafiri wakoloni walileta msiba mwingine wa kuumiza. Wakawapa Mayahudi dola katika Ardhi Iliyobarikiwa, mahali pa Israa (safari ya usiku), na asili ya Miraaj (kupaa) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw). Kisha wakawapa njia za kuishi. Kubwa zaidi katika njia hizo ni kulinda usalama wake kupitia watawala vibaraka wanaoizunguka. Kwa hivyo wakashindwa na Mayahudi katika kila vita vilivyotokea, mpaka wakaipa dola ya Kiyahudi sura nyengine isiyokuwa ile sifa ambayo Mwenyezi Mungu (swt) amewasifu kwayo: ﴿وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ﴾ **"na wamepigwa na unyonge."** [Surah Aali Imran 3: 112]. Na watawala hawa hawakuridhika na hilo pekee. Badala yake, walifanya jitihada zote za kuibadilisha kadhia hiyo kutoka kuondolewa kwa umbile la Kiyahudi, hadi kujadiliana nayo, kwa ombi kwamba ingejiondoa kutoka kwa baadhi tu ya yale maeneo waliyoyakalia kimabavu mwaka wa 1967!

Zaidi ya hayo, dola ya Mayahudi ilikuwa, na bado ingali inatenda jinai mbaya sana nchini Palestina. Mauaji ya Jenin, mnamo tarehe 26 Januari 2023, yanashuhudia hilo. Jeshi la umbile la Kiyahudi, likiwa na vikosi vikubwa na vyenye silaha nzito, lilivamia kambi ya Jenin, na kutekeleza mauaji makubwa ambapo watu tisa waliuawa shahidi. Wakati huo, walitekeleza uhalifu mbaya zaidi kupitia kuua, kubomoa kuta juu ya waliojeruhiwa, na kukanyaga kwa matingatinga. Kisha likaendelea na uchokozi wake dhidi ya Nablus, kuivamia Kambi ya Aqabat Jaber, kuua na kujeruhi, na kusababisha mashahidi na majeruhi… na yote haya yalitokea bila ya watawala katika Ardhi za Kiislamu kuhamasishana kuwaokoa. Badala yake, mfano bora zaidi wao ni yule ambaye alitoa upatanishi wake kati ya mhalifu na mhasiriwa aliyetendewa uhalifu. Mwenyezi Mungu awaangamize; wanadanganyika vipi? Na wanafanyaje zaidi ya hayo huku wakikimbilia kufanya uhalifu wa kuhalalisha mahusiano na Mayahudi? Baada ya watawala wa Misri kuongoza maandamano haya ya udhalilishaji na fedheha, PLO na kisha watawala wa Jordan, Imarati, Bahrain na Morocco mtawalia, wote walifuata mkondo huo. Na hii hapa Sudan inawafuata katika uhalifu huo kwani Rais wa Sudan, Al-Burhan, alikutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kiyahudi Eli Cohen jijini Khartoum mnamo tarehe 2 Februari 2023 kujadili uhalalishaji mahusiano! Hakuna hata mmoja wao anayejali udhalilifu unaowazunguka. ﴿سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ﴾ **"Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya."** [Surah Al-Anaam 6:124].

Kwa hakika ni ajabu kwamba kwa kila ongezeko, au kila uhalifu unaotendwa, na umbile la Kiyahudi, viongozi wake, siku moja kabla au siku hiyo hiyo, wako mikononi mwa watawala wa Kiarabu, au kwenye ziara kwao. Kabla ya uhalifu dhidi ya Jenin, Netanyahu alikuwa mgeni katika kasri la utawala wa Jordan! Wakati wa uhalifu dhidi ya Jenin, Mamlaka ya Palestina ilikuwa ikiratibu usalama na Mayahudi, kwa kukubali kwake yenyewe kwa sababu ilidai kwamba ingesitisha uratibu wa usalama, baada ya uhalifu huo. Hivyo, ndivyo ilivykuwa! Hata hivyo, cha kustaajabisha na kushangaza zaidi ni kwamba, pindi mmoja wa mashujaa wa Palestina alipoilinda ardhi yake na watu wake, na kuwaua Mayahudi saba katika operesheni ya Al-Quds, baada ya mauaji ya Jenin, watawala katika nchi za Kiislamu walikimbilia kulaani! Wizara za mambo ya nje za Uturuki, Imarati, Jordan na Misri, zote zililaani operesheni ya Al-Quds katika taarifa kwa vyombo vya habari!

Sasa, sio Palestina pekee iliyochomwa kisu mgongoni na watawala hawa bali pia walikubali au kuyasalimisha, maeneo mengine matukufu ya ardhi ya Uislamu. Kashmir iliunganishwa kwa nguvu na washirikina wa Kibaniani, katika dola yao, huku watawala wa Pakistan wamekaa kimya ... Waislamu wa Rohingya wanachinjwa huko Myanmar (Burma), huku watawala wa Bangladesh ni kana kwamba wamelala, bila kuona ... kisha kuna Turkistan Mashariki, ambapo China inafanya mauaji makubwa, huku dola za sasa katika Ardhi za Kiislamu zikidumisha kimya kama kimya cha makaburi. Kila wanapozungumza kuhusu mauaji hayo hudai kuwa ni mambo ya ndani ya China! ﴿كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ إِنْ يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا﴾ **"Ni neno kuu hilo litokalo vinywani mwao. Hawasemi ila uwongo tu."** [Surah Al-Kahf 18:5].

Kisha makafiri wakoloni hawakuridhika na fedheha waliyoufanyia Ummah. Badala yake walikiuka imani yake. Hivyo yule mtu duni aliyepitiliza mipaka alichoma nakala ya Quran Tukufu mbele ya jengo la ubalozi wa Uturuki, jijini Stockholm, mnamo Jumamosi 21 Januari 2023, baada ya mamlaka ya Uswidi kuruhusu hilo... Kisha uhalifu wao ukaendelea hadi kuchomwa kwa Qur'an Tukufu huko The Hague na kisha Copenhagen mnamo Ijumaa, 27 Januari 2023. Baadaye, tuliitazama Al-Azhar, kupitia Mwangalizi wake wa Al-Azhar wa Kupambana na Misimamo mikali, ikitoa taarifa yenye maneno makali ya kulaani na kutaka kusimama kupinga majaribio ya kukiuka matukufu ya kidini. Hapana shaka kwamba Wanazuoni wa Al-Azhar wanajua kwamba jibu la kuchomwa moto kwa Qur'an Tukufu si laana ya maneno tu, bali ni lazima majeshi yakusanywe kunusuru Kitabu cha Mwenyezi Mungu (swt) na Dini yake. Kuchoma moto Qur'an Tukufu ni tangazo la vita dhidi ya Umma wa Kiislamu na imani yake. Kwa hiyo, jibu ni vita vinavyotoa mfano kuogofya kwao, ili kuwazuia wengine. Amesema Mwenyezi Mungu (swt),

***Endelea... UK 5***

﴿فَإِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِمْ مَنْ خَلْفَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ﴾ **“Basi ukiwakuta vitani wakimbize walio nyuma yao ili wapate kukumbuka.”** [Surah Al-Anfaal 8: 57].

**Enyi Waislamu:** Uchokozi dhidi ya Waislamu haukabiliwi kwa maneno ya mapambo kwa ajili ya kuonekana, kauli tupu zisizonufaisha wala kukidhi haja. Badala yake uchokozi unajibiwa kwa makali ya upanga, kwa mapigo yanayomfanya adui asahau minong'ono ya Shetani. Hivi ndivyo walivyokuwa Waislamu walipokuwa na Khilafah, na mwenendo wa matukio katika utawala wao unazungumzia pakubwa hilo. Huu ni ukweli uliothibitishwa kwamba hakuna mtu mwenye macho na ufahamu anayeweza kukataa. Mifano yake ipo katika historia ya Waislamu ambayo imepokewa katika (kitabu cha) “Mwanzo na Mwisho” (*Al-Bidaya wa Al-Nihaya*) cha Ibn Katheer, “Ufunguzi wa Ardhi” cha Al-Baladhuri, “Historia” cha Ibn Khaldun na “Historia ya Uislamu” cha Al-Dhahabi, miongoni mwa vyanzo vyengine. Sasa nawanukulia kutoka kwao:

“Kisha ukaja mwaka wa 87 baada ya Hijrah... ndani yake Qutayba ibn Muslim akafungua Poykent, ambayo ni moja ya wilaya za Bukhara... na haikufika adhuhuri Mwenyezi Mungu (swt) aliwapa ushindi... Yule aliyewashambulia Waislamu alikuwa mtu mwenye jicho moja, kutoka miongoni mwao. Alipokamatwa, alisema, “Ninajikomboa kwa mavazi elfu tano ya Kichina, ambayo thamani yake ni maelfu kwa maelfu.” Hivyo makamanda wakamshauri Qutayba kukubali hilo kutoka kwake. Qutayba akasema, "Hapana, Wallahi, kamwe hutatia hofu kwa Muislamu tena." **Kisha akaamrisha kuhusiana naye na shingo yake ikakatwa…**”

“Kisha ukaja mwaka wa 90 baada ya Hijrah... ndani yake Raja Dahir, mtawala wa Sindh, aliishambulia meli iliyokuwa imebeba wanawake wa Kiislamu, na kuwachukua mateka. Hivyo Khalifa alituma risala kwa wali (gavana) wake ili kulipiza kisasi kwa dhalimu huyo. Hivyo Muhammad bin Al-Qasim aliongoza jeshi na k**uwaokoa wanawake wa Kiislamu, akalipiza kisasi kwa mtawala huyo dhalimu na akaiteka ardhi ya Sindh**.”

“Kisha ukaja mwaka wa 223 baada ya Hijrah, na Mfalme wa Byzantino akaenda kwenye Ardhi za Waislamu, akiwaua na kuwateka nyara watu wa Zabtara. Mwanamke mmoja akapaza sauti, “Ewe Mu’tasim, uko wapi.” Wito huu ulimfikia Khalifa al-Mu’tasim, ambaye alijibu, “Niko kwenye huduma yako.” Yeye binafsi aliongoza jeshi na kulipiza kisasi kwa mwanamke huyo. Aliuliza ni ipi kati ya ardhi za Byzantino ilikuwa kubwa zaidi. Aliambiwa kwamba ilikuwa Amuriyya, ambayo ilikuwa "karibu na Ankara." Kwa hiyo akaifungua.”

“Kisha ukaja mwaka wa 582 baada ya Hijrah... ndani yake Arnat (Raynald), mvamizi wa Al-Karak, kwa khiyana alifunga njia, kwa ajili ya msafara mkubwa wa Mahujaji, ambao ulitoka Misri ambaye aliwaua na kuwateka nyara. Hivyo Sultan Salah ud-Din alijiandaa kwa ajili ya vita. Aliomba askari kutoka nchini. Aliapa kwamba kama angemshinda Arnat, angemuua. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu akamjaalia kuwa mshindi katika mwaka wa 583 baada ya Hijrah, katika Vita vya Hattin, katikati ya Rabi’ Al-Akhir. **Kisha Salah Al-Din akamuua Arnat, kwa mkono wake mwenyewe, kama adhabu kwa ajili ya khiyana yake na kuziba njia**. Hapo ndipo ukombozi wa Al-Aqsa ulipotokea, mnamo tarehe 27 Rajab, 583 baada ya Hijrah.”

“Kisha mwaka 1307 baada ya Hijrah, mwaka 1890 M, mtunzi wa skripti iliyomkashifu Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), akajaribu kuionyesha kama mchezo wa kuigiza, katika moja ya kumbi za sinema jijini Paris. Khalifa Abdul Hamid alipopata habari hii, alimwita balozi wa Ufaransa jijini Istanbul na akakutana naye kwa makusudi akiwa amevalia sare za kijeshi. Kisha akamtishia kwamba ikiwa itaonyeshwa, Dola la Kiuthmani itatangaza kukata uhusiano na Ufaransa, katika hali ya vita. Akamwambia kwa sauti ya ukali, akisema, **"Mimi ni Khalifa wa Waislamu ... nitageuza ulimwengu juu ya vichwa vyenu, ikiwa humtausitisha mchezo huu."** Ufaransa ilijibu kwa kuzuia mchezo huo kuonyeshwa…”

Makafiri wakoloni walikuwa wakijua, wakati huo, kwamba ukiukaji wowote wa matukufu ya Uislamu, na Waislamu, ungekabiliwa na kukatwa ndimi na kuvunjwa viungo... Leo hii Quran Tukufu, Mtume (saw) na Ardhi za Waislamu zinashambuliwa, wakati uchokozi haulipizwi kisasi!

Hii ni kwa sababu tu hakuna Imam, Khalifa Rashid (Khalifa Muongofu), anayeulinda Ummah kutokana na shari za maadui. Imepokewa katika Hadith iliyo sahihi iliyopokewa na Bukhari na Muslim, kwamba amesema (saw): «إِنَّمَا الْإِمَامُ جُنَّةٌ، يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ، وَيُتَّقَى بِهِ» **“Imam ni ngao, watu hupigana nyuma yake, na hujihami kwake.”** [Bukhari na Muslim]

**Kwa kutamatisha, narudia ombi langu kwenu, Enyi watu wenye nguvu na ulinzi...** Nyinyi pekee ndio mnaoweza kuuponya moyo wa Ummah kutokana na maadui zake, maadui wa Dini yenu. Nyinyi pekee ndio mnaoweza kukomesha udhalilifu uliowafikia Waislamu katika ardhi zao... Basi inukeni kutekeleza wajibu wenu, Mwenyezi Mungu (swt) awabariki. Inukeni ili mutupe Nusrah yetu, Nusrah kwa Hizb ut Tahrir ili kusimamisha Khilafah Rashida. Sio tu njia pekee ya ushindi katika hali halisi ya sasa. Badala yake, ni kwa sababu ni faradhi kubwa ya kwango cha kwanza.

***Endelea... UK 6***

Kwanza, yeyote asiyefanya kazi na hali ana uwezo wa kusimamisha Khilafah, na kusimamisha Khalifah anayestahiki Bayah (ahadi ya utiifu), basi dhambi lake ni kubwa kana kwamba amekufa kifo cha kabla ya Uislamu (Jahilliyah), ikidhihirisha ukali wa madhambi kama alivyo sema, «وَمَنْ مَاتَ وَلَيْسَ فِي عُنُقِهِ بَيْعَةٌ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً» **"Na atakaye kufa ilhali hana bay'ah (ahadi ya utiifu kwa Khalifa) shingoni mwake, amekufa kifo cha kijahiliya."** [Muslim]. Pili, Waislamu walichukua kiapo cha Bayah kwa Khalifa, kabla ya kuanza maandalizi mazishi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) na kutekeleza wajibu wa mazishi yake. Yote hayo yanatokana na umuhimu wa Khalifah. Tatu, Umar (ra) siku ya kifo chake, aliweka kikomo cha muda, cha siku tatu na si zaidi, kwa ajili ya kumchagua Khalifa miongoni mwa wale sita waliopewa bishara ya Pepo. Ikiwa hakuna makubaliano yaliyofikiwa kuhusu Khalifa, ndani ya kipindi hicho, basi mpinzani alipaswa kuuawa. Hili lilikuwa ni katika ijmaa ya Maswahaba (ra) ambao hakuna uovu wowote ulioripotiwa kuwahusu. Hivyo, ilikuwa ni Itifaki ya pamoja ya Maswahaba (ra). Hata hivyo, kwetu sisi, "siku tatu nyingi" zimepita juu yetu! Hakika kusimamisha Khilafah ni jambo kubwa.

**Enyi Wanajeshi wa Mwenyezi Mungu:** Tunatambua kwamba Malaika hawatashuka kutoka mbinguni ili kutusimamishia Khilafah. Bali Mwenyezi Mungu (swt) atatuteremshia Malaika watusaidie tu ikiwa tutafanya kazi kwa bidii katika kusimamisha Khilafah. Ni ahadi iliyothubutu katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ﴾ **"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao."** [Surah An-Nur 24:55]. Ni bishara njema ya izza, baada ya utawala huu wa kidhalimu, katika hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt), «ثُمَّ تَكُونُ مُلْكاً جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ» **"…Kisha utakuwepo utawala wa kutenza nguvu, na utakuwepo katika muda upendao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa apendapo kuuondoa. Kisha itakuwepo Khilafah kwa Njia ya Utume."** Kisha yeye (saw) akanyamaza. [Imepokewa na Ahmad]. Pia tunatambua kwamba maadui wa Uislamu wanaona kusimamisha tena kwa Khilafah ni jambo lisilowezekana. Wanarudia kauli ya wafuasi wao kutoka miongoni mwa wanao kejeli, ﴿غَرَّ هَؤُلَاءِ دِينُهُمْ﴾ **"Watu hawa dini yao imewadanganya."** [Surah Al-Anfal 8:49]. Lakini kama vile msemo huo ulivyokuwa laana kwa wale waliotangulia kuusema, kwani Mwenyezi Mungu ameitukuza Dini yake na akawapa ushindi watu wake, ni laana kwa wale wanaousema leo, kwani Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima, yuko pamoja na waja wake wenye ikhlasi wanaofanya kazi kwa bidii, bila ya kutoka katika nyoyo zao na viungo vyao, kauli ya Mwenyezi Mungu (swt), ﴿إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً﴾ **"Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake."** [Surah At-Talaq 65:3]. Kila uchao, wanakaribia kwenye Qadr "azma," hii kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu (swt). ﴿وَيَقُولُونَ مَتَى هُوَ قُلْ عَسَى أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا﴾ **"na watasema: Lini hayo? Sema: A'saa yakawa karibu!"** [Surah Al-Israa 17:51].

Wa Alaikum Assalaam wa Rahmutallahi wa Barakaatahu

**Ndugu Yenu, Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah,** **28 Rajab 1444 H**

**Amiri wa Hizb ut Tahrir** **19 Februari 2023 M**

# Majanga ya Kimaumbile yanazidi kuwa mabaya kwa kukosekana Khilafah



**Habari:**

Ripoti ya habari ya CNN siku 5 baada ya tetemeko la ardhi la Uturuki kuonya juu ya maafa makubwa zaidi nje ya kuporomoka kwa awali kwa miundombinu katika maeneo yanayopakana na Syria. Hali ya hewa ya baridi na mvua pamoja na uhaba wa chakula, vifaa vya matibabu na maji vinavyoingia katika eneo hilo inamaanisha wengi watakufa ovyo. Makaazi ni sababu kuu inayoathiri viwango vya manusura walio katika hatari ya kushuka kwa kiwango cha joto mwilini (hypothermia) katika hali ya baridi kali. **Wasyria wako hatarini haswa kwani UN imeshikilia kura ya TURUFU juu ya msaada unaoingia katika maeneo yaliyoathirika**. Urusi na China zimetumia nafasi zao kuziba vivuko 3 kati ya 4 vya kuingia katika mpaka wa Syria na kukwamisha kwa kiasi kikubwa misaada ambayo inaweza kutolewa kwa maelfu ya wanawake na watoto waliokosa makaazi na tayari rasilimali zinazopatikana kwao ni finyo.

**Maoni:**

Wazo la kwamba umbile lisilokuwa la Kiislamu ndilo linalosimamia iwapo Waislamu watapokea usaidizi wa kubadilisha maisha au la ni hali iliyoharamishwa na haikubaliwi na Mwenyezi Mungu (swt).

Idadi ya manusura tayari ni ya kimiujiza huku watu wengi zaidi wakiwa wamekufa kuliko wale waliotoka kwenye majengo yaliyoporomoka. Kufikiri kwamba baada ya yote ambayo wamevumilia kwa kweli wangekufa kutokana na kitu ambacho kilikuwa kinaweza kuzuiliwa kabisa ni jambo la kutisha zaidi kuliko tetemeko la ardhi lenyewe.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Geneva, meneja wa kukabiliana na matukio wa WHO Robert Holden alionya kuwa kuna "...watu wengi" wanaoishi "nje ya makaazi, katika hali mbaya na za kutisha. Tumepata mkatiko mkubwa wa usambazaji wa maji, tumepata mkatiko mkubwa wa mafuta, vifaa vya umeme, vifaa vya mawasiliano, mambo msingi ya maisha. Tuko katika hatari halisi ya kuona maafa ya pili ambayo huenda yakasababisha madhara kwa watu wengi zaidi kuliko maafa ya awali ikiwa hatutasonga kwa kasi na nguvu kama vile tunavyofanya katika upande wa utafutaji na uokoaji."

Ukubwa wa changamoto hiyo unazidishwa na ukweli kwamba maeneo yaliyoathiriwa nchini Uturuki na Syria yanakabiliwa na baridi zaidi kuliko joto la kawaida. Kwa mfano, mji wa Syria wa Aleppo unatabiriwa kuwa na viwango vya chini vya -3°C hadi -2°C (27°F hadi 28°F) mwishoni mwa wiki hii, ilhali viwango vya chini vya Februari kwa kawaida huwa joto zaidi.

Siku 4 baada ya tetemeko la ardhi, kivuko cha Bab al-Hawa - njia pekee ya misaada ya kibinadamu kati ya Uturuki na Syria kiliruhusiwa kufunguliwa. "Je, inakuwaje barabara ziko sawa kwa magari yanayobeba miili, lakini sio kwa msaada?" Mazen Alloush, msemaji aliyeghadhabishwa wa Bab al-Hawa alikuwa ameiuliza CNN. Abu Muhammad Sakhour, mfanyibiashara wa zamani, anajitolea kama muuguzi katika mji unaodhibitiwa na waasi wa Idlib, akifunga majeraha kwa wahasiriwa wa tetemeko la ardhi na kuwafanyia uchunguzi majeruhi ambao wameruhusiwa kutoka katika hospitali zilizojaa watu.

"Hali ni mbaya kweli kweli," alisema. "Sasa tunaponya majeraha yetu wenyewe." Kwa walio hatarini kama vile wanawake wajawazito, wazee, watoto wachanga na wadogo, masaa yanayotumiwa katika hali kama hizi yanaweza kutosha kusababisha vifo kutokana na kuanikwa baridini na udhaifu.

Jambo hili la uhai na kifo ni jambo ambalo haliwezi kujadiliwa au kuachwa kwenye mikono ya kura zinazopigwa na maadui wa Uislamu. Kiukweli kile kinachotokea hapa ni uovu wa mataifa kupiga kura iwapo watu wataishi ili wafe. Khilafah na kiongozi wa Uislamu kamwe hangekubali ulisia kama huo kutokana na uwajibikaji wake wa kutuma msaada kwa watu wote katika eneo hilo, wakiwemo raia wasiokuwa Waislamu. Hakuna kisingizio kinachoweza kutolewa cha kutosimamisha tena Khilafah kama jambo la dharura la haraka kabla ya maafa mengine ya kimaumbile kutokea na Ummah wetu kuachwa na dua kwa Mwenyezi Mungu (swt) pekee!


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Imrana Mohammad**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Ajenda na Genge la (LGBTQ) ni Matunda Mabovu ya Mfumo Muovu wa Kirasilimali

Januari 6 mwaka huu mwili wa Edwin Chiloba mwenye umri wa miaka 24 mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Eldoret, ulipatikana ndani ya sanduku ukiwa umeshindiliwa vitambara mdomoni na puani mwake. Kifo chake kimezuwa gumzo ndani na nje ya nchi haswa katika vyombo vya habari na katika mitandao ya kijamii kwa sababu Chiloba ni mtetezi wa LGBTQ+ (usago, ukhanithi…). Msemaji wa wizara ya kigeni ya Amerika Ned Price alitangaza tarehe 10 kuwa serikali ya Biden itatoa usaidizi kwa serikali ya Kenya kuchunguza mauaji hayo kwa kisingizio cha ukiukaji wa haki za kibanaadamu.

Ndani ya mwavuli wa haki za Kibinadamu, Wakoloni wamagharibi wanaeneza uchafu wa usago, ubasha na uhanithi LGBT (Lesbian Gay Bisexual Transgender). Marekani, nchi iliyohalalisha  ufuska wa ndoa za jinsia moja mwaka 1999, kulifanyika maandamano  mwaka 1965-66 ya jamii ya mashoga wakitaka kutobaguliwa kama raia wa daraja la pili na hii ni baada yao wao kuzusha rabsha na polisi huko Stonewall. Mwongo mmoja uliopita Baraza la kimataifa la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa likapitisha rasmi azimio lake la kutambua rasmi "haki" za LGBT. Nalo shirika la Amnesty International linashikilia msimamo huo sambamba na miungano ya mawakili katika mataifa mbalimbali duniani iko kifua mbele kutetea uovu huu.

Kufikia Novemba mwaka jana tayari Mataifa 30 yamehalalisha rasmi uovu huu unaongamiza vizazi. Bara la Afrika ambapo hadi sasa mataifa mengi yake hayajatambua ama kuhalalisha LGBT, ukiachilia mbali Afrika Kusini, lipo katika shinikizo la mataifa makubwa ya kibepari yanayotumia njia za kiuchumi, kisiasa na hata kijamii kulazimisha uchafu huu. Kwa masikitiko makubwa mashirika kama vile USAID na DANIDA yanayotumika kueneza maovu haya yamepewa ruhusa kufanya kazi katika nchini nyingi barani chini ya kisingizio cha kutoa misaada. Filamu za LGBT zinapeperushwa kama ile ya iliyopigwa marufuku nchini Kenya “I am Samuel’ iliyozinduliwa mwaka 2020.

Kukuza na kushajiishwa kwa hulka hii mbovu kunatokana na ufahamu wao wa kipotofu na mawazo yao ya kihuria/ uhuru (liberal views) kwamba kukidhi matamanio ya kimwili ndiko kufaako kupewa kipaumbele zaidi hata kuliko kuendeleza kizazi. Kwa kile wakiitacho uhuru wa kibinafsi, jamii zao huruhusiwa kufanya kitendo chochote kile maadam kitafikia kwenye raha. Na ni kwa muktadha huu ndio tumefikishwa hapa ndoa za masago na mabasha! Ni wazi kuwa haki za LGBT zinalindwa na mfumo muovu wa Kimagharibi.

**Enyi Waislamu:** Tambueni kwamba wakoloni wa Kimagharibi wamekwisha angamiza kizazi chao na sasa wamo mbioni kuhujumu familia zenu kuzifanya kama wanyama bali zaidi ya wanyama! Kampeni ya LGBT inalenga mmomonyoko wa kimaadili na kukatisha mahusiano mazuri katika wanaume na wanawake. Kejeli nyingi mtafanyiwa na Wamagharibi kwa sababu ati nyinyi mnabeba msimamo wa kwamba ndoa pekee inayotambulika kisheria ni baina ya mwanamume na Mwanamke wala sio mashoga au masago! Hata hivyo, mtasimangwa na kukejeliwa na Wamagharibi na makundi yao kama harakati za wanawake (Feminists). Lengo la kejeli na masimango haya dhidi yenu ni nyinyi muanze kuyakubali machafu haya au kwa uchache mkubali na kutambua haki zao’. Na sio ajabu pia mkapachikwa majina ya ugaidi na misimamo mikali kwa sababu ya kupinga maovu haya.

Waenezaji uchafu huu hata wakiambiwa; “Acheni kuleta uharibifu katika jamii”, majibu yao ni kama alivyosema Mwenyezi Mungu (swt) “Laa bali sisi ni watengenezaji mambo!” Na wakiambiwa muogopeni Mwenyezi Mungu kwa kukomeka na madhambi haya kwa inadi wao wanaendelea kuhimiza watu kufanya machafu hayo. Wakoloni wanajua vyema kwamba nyinyi munachukizwa na machafu haya na kwa nini msichukizwe ilhali munatambua vyema Jinsi Mwenyezi Mungu (swt) alivyoangamiza watu wa Nabii Lut (as):

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا جَعَلْنَا عَالِيَهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِنْ سِجِّيلٍ مَنْضُودٍ

**“Basi ilipofika amri Yetu, Tukaifanya juu yake kuwa chini yake, na Tukawapigia mvua ya changarawe za udongo mgumu zipandanazo.”** [11:82].

**Enyi Wanaume wa Kiislamu:** Nyinyi ndio wasimamizi wa familia zenu (wake zenu na watoto wenu) asema Mwenyezi Mungu (swt):

ٱلرِّجَالُ قَوَّٰمُونَ عَلَى ٱلنِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَآ أَنفَقُوا۟ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ ۚ فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٌ لِّلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُ

**“Wanaume ni Walinzi wa Wanawake kwa sababu Mwenyezi Mungu amewafadhili baadhi yao kuliko wengine, na kwa sababu ya Mali zao walizozitoa basi wanawake wema ni wale wenye kutii wanaohifadhi (hata) wasipokuwapo waume zao yale Aliyoyahifadhi Mwenyezi Mungu.”** [4:34]

Usimamizi huu sio udikteta juu ya familia zenu bali ni usimamizi wa kimajukumu ili kuhakikisha kiwango cha juu cha kimaadili bali mshikamano thabiti baina ya wanafamalia. Usimamizi huu uko ndani ya Uislamu

***Endelea... UK 9***

pekee wala haupatikani ndani ya mfumo batili wa Kimagharibi wa Kibepari uliomfanya mwanadamu afukuzane na matamanio yake kama mnyama hivyo kuhujumu mahusiano baina ya wanaume na wanawake. Natija ya mfumo huu ni kuziona familia zilizo paraganyika kukiwa hakuna huruma ya baba kwa mwanawe huku mwana kutomhurumia babake, mke kutoheshimu mumewe na mume kutoheshimu mkewe!

**Enyi Waislamu:** Tunawajibika kupaza sauti zetu katika kupinga matendo haya maovu, kufafanua umuhimu wa taasisi ya ndoa zetu, mahusiano baina ya wanaume na wanawake yote kwa mtazamo wa mfumo wetu wa Uislamu. Tuungane na Hizb ut Tahrir harakati ya Kiislamu inayofanya kazi ya kuhuisha maisha mema ya Kiislamu kupitia kusimamisha dola ya Khilafah kwa njia ya Utume katika mojawapo ya nchi za Waislamu. Dola hii ndio itakayolinda jamii kikamilifu dhidi ya maovu yote.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسْتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

**"Enyi Mlioamini Muitikieni MwenyeziMungu na Mtume wake anapokutieni katika yale yatakayokupeni uhai mzuri wa duniani na Akhera."** [8:24].

**H. 19 Rajab 1444** **Hizb-ut-Tahrir**

**M. : Ijumaa, 10 Februari 2023** **Kenya**




 Pepe: info@uqab.or.ke

# Enyi Waislamu, Komesheni Machafuko Duniani kwa Kuwa na Tawakkul kwa Mwenyezi Mungu (swt) na Shariah Yake na Fanyeni Kazi kwa ajili ya Khilafah

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Sarah Mohammed – America**



Tangu kuvunjwa kwa Khilafah mwaka 1924, kila kona ya dunia imekuwa katika machafuko ya kuendelea. Hii ni licha ya kuwa kumekuwa na maendeleo katika teknolojia, matibabu, kilimo, jeshi, na inaonekana maendeleo katika siasa na katika kujenga haki sawa kati ya jinsi na jinsia. Tumehadaiwa katika kuamini kwamba mfumo ule ule unaotuambia kwamba hatuhitaji kutazama Quran na Sunnah (yaani, kutenganisha kanisa na dola), bali kwenda kwa mfumo uliobuniwa na mwanadamu (yaani, demokrasia) unaoegemezwa juu ya matamanio ya mwanadamu, na mfumo wa kiuchumi (yaani, ubepari) unaoegemezwa juu ya riba unaoweka wingi wa mali mikononi mwa wachache kuongoza mambo yetu yote ya maisha. Tunapaswa kukaa chini na kutafakari kwa nini machafuko haya yote yanatokea kwa kuendelea na kwa kila jaribio la "kuyasuluhisha", mambo yanazidi kuwa mabaya, au migogoro mipya inaundwa bila kujali ni kiasi gani cha maendeleo tunachoonekana kufanya. Kwa uchunguzi wa kina, inakuwa dhahiri kwamba migogoro hii siyo ya kimaumbile, bahati mbaya, au kiasili kutokea katika jamii, lakini kwa kubuniwa na wale waliochukua udhibiti wa dunia na kuulazimisha mfumo wa ubepari wa kisekula kutoka Mashariki hadi Magharibi.

Katika ulimwengu wa Kiislamu, ngao yetu ilipochukuliwa, tulilazimishwa kuishi chini ya madikteta wakatili, wafalme haramu, marais na mawaziri wakuu. Tulilazimishwa kuishi chini ya umaskini uliokithiri, ubadhirifu na wizi wa maliasili, kuvunjwa kwa taasisi za elimu na matibabu ambazo hapo awali zilikuwa vituo vya maendeleo na huduma bora za afya, kusambaratika kwa mahusiano kati ya mume na mke; wazazi na watoto kupitia kuanzishwa kwa ufeministi, ubinafsi, na LGBTQ+, vurugu za mara kwa mara, na janga la wakimbizi lisilokwisha ambalo limetusibu tangu tulipogawanywa katika dola za kitaifa. Walituondolea macho yetu ya jinsi ya kuendesha mambo yetu ya maisha kwa kubadilisha fahamu ya kibepari ya manufaa na madhara badala ya halali na haramu.

Hata hivyo, hata nchini Marekani, pamoja na nguvu zake zote, pesa, na sheria zinazobadilika kila mara zinazokusudiwa kuwa jumuishi na zilizoendelea; machafuko na migogoro kamwe haimaliziki. Licha ya kilio cha umma na maafisa wa serikali juu ya George Floyd, watu weusi nchini Marekani bado wanauawa na kufungwa kwa idadi kubwa zaidi kuliko jinsi nyengine yoyote, au kabila lolote. Licha ya ahadi za Biden na Wanademocrat kuwasaidia wale wanaotaka kuepuka umaskini na vurugu kuishi nchini Marekani, wahamiaji bado wamefungwa katika magereza wanaokabiliwa na uhamisho. Licha ya vuguvugu la kutetea haki za wanawake, wanawake nchini Marekani bado wanakabiliwa na ukosefu wa usawa wa kipato, bado wanafanywa kuwa ni vyombo, wanakabiliwa na unyanyasaji wa kijinsia uliokithiri, na wako katika hatari kubwa ya kuishi katika umaskini pamoja na watoto wao. Licha ya sheria za kumiliki bunduki, Marekani ina kiwango cha juu zaidi cha ghasia za bunduki miongoni mwa mataifa mengine tajiri ambazo zinazidi kuwa mabaya, kama inavyoonekana katika mojawapo ya matukio ya hivi punde ya ufyatuaji risasi shuleni ambapo mvulana wa miaka 6 alimpiga risasi mwalimu wake. Licha ya kuwa moja ya nchi tajiri zaidi duniani, uhaba wa chakula ni jambo la kawaida kwa Wamarekani milioni 34, pamoja na, wengine ambao hawana mifereji ya

***Endelea... UK 11***

ndani, upataji elimu, huduma za afya, na maji safi! Licha ya kutangazwa kuwa kinara wa usawa na demokrasia, taifa lilishuhudia maasi maarufu ya mwaka 2021 ambayo yalifichua hali ya kutoridhika na migawanyiko iliyokuwepo ndani ya jamii.

Je, huyu ndiye tunayepaswa kumwangalia ili atuongoze? Je, hii sio ishara kwetu kwamba kuishi chini ya sheria zilizotungwa na mwanadamu hakutatuletea chochote isipokuwa machafuko na kiwewe?

Tunawezaje kuendelea kutazama demokrasia, ubepari na usekula ili kutatua matatizo yetu na ilhali Mwenyezi Mungu (swt) ametupa hukmu na ramani ya namna ya kuitabikisha kama ilivyowekwa na kipenzi chetu Mtume Muhammad (saw) alipoasisi dola mjini Madina? Ingawa inaweza kuonekana kana kwamba ni kazi kubwa, ni lazima tupate kishajiisho kutoka kwa Mtume wetu (saw) na Maswahaba (ra) pindi walipokabiliana ana kwa ana si tu na makabila madogo ya kipagani, bali na dola kuu za wakati huo; Warumi na Wafursi, ambao walikuwa bora zaidi kwa idadi na teknolojia ya kijeshi. Hata hivyo, kile ambacho Waislamu walipungukiwa nacho katika idadi na teknolojia, walikifidia kwa kitu chenye nguvu zaidi; Imani na Tawakkul kwa Mwenyezi Mungu (swt). Na Mwenyezi Mungu (swt) akawapa ushindi juu ya madhalimu wa zama zao. Waliitazama dunia kupitia kioo cha Uislamu na kilichowaongoza katika maamuzi yao ni kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu (swt). Hivi ndivyo walivyoweza kupiga hatua kubwa katika kueneza Uislamu kupitia utabikishaji wa Shariah na jihad fisabilillah kupitia dola ya Khilafah.

Ni lazima tuzingatie mafunzo haya na kama vile Maswahaba (ra) walivyofanya, tufikirie imani yetu kwa Mwenyezi Mungu (swt) na tukinai kwamba ni kupitia kumwamini Yeye pekee ndipo tutaweza kufanya mabadiliko ya kweli yanayohitajika kwetu kuleta utulivu na utulivu duniani. Kupitia Shariah, tuliyotumiwa na Muumba wetu, tunazo sheria kamilifu na zinazotosha kutatua mambo yetu yote na jaribio lolote la kutafuta hukmu kutoka kwa kitu chochote nje ya Shariah yake ni mtego wa Shetani ili atupoteze. Mwenyezi Mungu (swt) ametupa neema zake kwa kutukamilisha Dini yake na kutufanya kuwa mashahidi kwa wanadamu kama vile Mtume Muhammad (saw) alivyokuwa shahidi juu yetu.

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَـٰكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِّتَكُونُوا۟ شُهَدَآءَ عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيدًا

**“Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani, ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu.”** [Al-Baqarah:143]

Tunahitaji kujiangalia zaidi ya nafsi zetu kama watu binafsi na kukumbuka kwamba Mwenyezi Mungu (swt) aliituma Quran yake na Shariah yake kama rehma kwa wanadamu. Hili linauhitaji Umma wa Muhammad (saw) kujihuisha wenyewe kupitia imani yake thabiti kwa kurudisha mfumo kamili wa maisha wa Kiislamu kupitia kusimamisha tena Khilafah. Dhihirisho la kivitendo la Shariah bila shaka litatumika kama mwenge wa nuru na njia ya uokozi kwa ulimwengu ambao umezungukwa na giza na machafuko ya Urasilimali. Kupitia dola ya Khilafah, yenye kusimama nyuma ya Khalifa mwadilifu, Umma utakuwa tayari kutumia rasilimali zake zote kuupeleka Uislamu ulimwenguni.

# Hizb ut Tahrir / Kenya Yaandaa Maandamano Baridi kwenye Kumbukumbu ya Miaka 102 ya Kuanguka kwa Khilafah











Pepe: info@uqab.or.ke